

HALMASHAURI YA WILAYA YA MADABA
MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI
CHA TAHEHE 28/11/2021

MAHUDHURIO

1. JOSEPH MRIMI	M/KITI
2. SHUKRAN K FARAJI	KATIBU
3. DR BETY MRAWALA	MJUMBE
4. ABDUL MANGA	MJUMBE MSHAURI
5. IDD MPONDA	MJUMBE

AJENDA ZAKIKAO

1. KUFUNGUA KIKAO
2. KUTHIBITISHA AGENDA
3. KUSOMA NA KUPITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA
4. KUWASILISHA MAPENDEKEZO YA KUTUMIA NJIA YA FORCE ACCOUNT KATIKA UTEKELEZA WA MANUNUZI YA MIRADI YA COVID KWA IDARA YA ELIMU.
5. KUFUNGA KIKAO

AGENDA NO 1 MDC/BZ/2021/2022 .KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alianza kwa kumkaribisha katibu wa kikao ili aweze kuelezea katika kikao cha bodi madhumuni makuu ya kikao hiki. Baada ya melezo hayo kutoka kwa katibu wa bodi mwenyekiti alifungua kikao saa 10:00 asubuhi.

AGENDA NO 2. MDC/BZ/2021/2022. KUTHIBITISHA AGENDA

Katibu alisoma agenda na wajumbe kwa pamoja waliridhia agenda zote

AGENDA NO 3. MDC/BZ/2021/2022. KUSOMA NA KUPITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA

Mwenyekiti alimkaribisha katibu wa BODI YA ZABUNI ili aweze kuwapitisha wajumbe katika muhtasari wa kikao kilichopita, katibu aliwapitisha na wote waliweza kuridhia muhtasari huo kuthibitishwa na kusainiwa ili uweze kuwa kumbukumbu halali kwa matumizi ya baadaye

AGENDA NO 4. KUWASILISHA MAPENDEKEZO YA KUTUMIA NJIA YA FORCE ACCOUNT KATIKA UTEKELEZA WA MANUNUZI YA MIRADI YA COVID KWA IDARA YA ELIMU.

Mwenyekiti alimkaribisha katibu ili aweze kuelezea bodi nini kinatakiwa kifanyikje ili kufanikisha jukumu ili nzito la ujenzi.

Katibu alianza kwa kusema, Ndugu wajumbe wa bodi ya manunuzi Halmashauri yetu imepokea jumla ya tsh 340,000.000/=(milioni mia tatu arobaini ili kuweza kutekeleza ujenzi wa madarasa 17 katika shule 7 za sekondari zilizopo ndani ya wilaya yetu.

Kazi hizo inaweza kufanyika kwa njia zaidi ya moja .ila kwakuwa miradi huiyo inatekelezwa katika mashule kwa upoande wa kitenngo cha manunuzi kinashauri njia ya force account ni njia bora kuweza kutumiaka katika utekelezaji wa miradi hiyo kwani serikali ya awamu ya sita imeonekana kufanya vizur katika njia hiyo pia njia hiyo ni nafuu kwani inaonekana kufanyika kwa gharama nzuri ukilinganisha na njia ya mkandarasi.hivyo swala ili limeletwa kwenu ili muweze kufanya maamuzi juu ya manunuzi haya ambayo yatahusisha manunuzi ya kumpata fundi na manunuzi ya vifaa na huduma mbalimbali za ujenzi.Pia ifahamike kuwa bodi ya zabuni ina mamlaka ya kuridhia au kuto ridhia kutumika kwa njia hiyo ya force account.

Mwenyekiti wa Bodi aliwauliza wajumbe kama kuna mtu yeyote ambaye anaweza kutaka ufafanuzi zaidi juu ya mapendekezo hayo ya kitengo cha manunuzi.

MAAZIMIO YA BODI YA ZABUNI

BODI YA ZABUNI imeridhia kazi ya hizo ziweze kufanyika kwa kutumia Force account mwenyekiti alisisitiza wataalamu wa kitengo pamoja na maafisa elimu kwa kushirikiana na waandisi wa halmashauri kuhakikisha wanatoa ushirikiano katika utekelezaji wa miradi hiyo na pia kila mmoja awajibike kwa nafasi yake kuhakikisha miradi hiyo inakamilika kwa wakati bila kuathiri matarajio ya viongozi wetu waliotupa jukumu la kusimamia miradi ya maendeo.Kwa maslai ya Taifa letu.

5.KUFUNGA KIKAO

Mwenyekiti aliahilisha kikao muda wa saa 10:00 jioni. Na kluwatakia kazi njeam wajumbe na kuwashukuru kwa mahudhurio mazuri.Na kumaliza kwa kutamka KAZI IENDELEE.

.....
KATIBU WA BODI YA ZABUNI
ZABUNI

.....
MWENYEKITI WA BODI YA

TAREHE.....28/11/2021